© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Amesema Allaah Subhanahu wa Ta'aalah (kama ilivyofasiriwa):

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. (Soorah az-Zaariyat 51:56).

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِى كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَٱجْتَنِبُوا۟ ٱلطَّٰغُوتَ ۖ

Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allaah, na muepukeni *Tâghût* . **(Soorah an-Nahl 16:36)**

۞ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّآ إِيَّاهُ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَٰنًا ۚ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ ٱلْكِبَرَ أَحَدُهُمَآ أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُل لَّهُمَآ أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾

Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa hishima.(Soorah al-Isra' 17:23)

وَٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ شَيْـًٔا ۖ

Muabuduni Allaah(Mwenyezi Mungu) wala msimshirikishe na chochote. (Soorah an-Nisaa 4:36)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

۞قُلْ تَعَالَوْا۟ أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ
شَيْـًٔا ۖ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَٰنًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوٓا۟ أَوْلَٰدَكُم مِّنْ إِمْلَٰقٍ ۖ نَّحْنُ
نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ وَلَا تَقْرَبُوا۟ ٱلْفَوَٰحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ وَلَا
تَقْتُلُوا۟ ٱلنَّفْسَ ٱلَّتِى حَرَّمَ ٱللَّهُ إِلَّا بِٱلْحَقِّ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمْ
تَعْقِلُونَ ﴿١٥١﴾

Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini. (Soorah al-An'am 6:151)

وَلَا تَقْرَبُوا۟ مَالَ ٱلْيَتِيمِ إِلَّا بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُۥ ۖ وَأَوْفُوا۟
ٱلْكَيْلَ وَٱلْمِيزَانَ بِٱلْقِسْطِ ۖ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۖ وَإِذَا قُلْتُمْ فَٱعْدِلُوا۟
وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۖ وَبِعَهْدِ ٱللَّهِ أَوْفُوا۟ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمْ
تَذَكَّرُونَ ﴿١٥٢﴾

Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka. (Soorah al-An'am 6:152)

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَٰطِى مُسْتَقِيمًا فَٱتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا۟ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن
سَبِيلِهِۦ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾

Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake (Soorah al-An'am 6:153)

Anasema Ibn Mas'ood (Radhiallaahu 'anhu) Anayetaka Kuangalia wasia wa Mtume **Muhammad (**Salla Allaahu alayhi wasalam) ambao una muhuri wake basi naasome kauli ya Allaah ta'aalah: **Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote --**mpaka **-- . Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. (Soorah al-An'am 6:151-153)**

Amesimulia Mu'aadh ibn Jabal (Radhiallaahu 'anhu): Nilikuwa juu ya punda nyuma ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) akaniambia : Ewe Mu'aadh **! wajua haki ya Allaah kwa viumbe vyake, na haki zao wao** ? Nikasema Allaah na Mtume wake ndio wajuao! Akaendelea : Haki ya Allaah kwa viumbe vyake ni **kumwabudu Yeye pekee bila ya kumshirikisha yeyote mwengine**. Ama haki ya viumbe ni **kutoadhibiwa asiyemshirikisha Allaah na chochote**; Nikasema Ewe Rasoolullaah! Kwa nini nisiwabashirie watu kwa hilo? Akajibu, Laa! Usifanye hivyo Wasije wakategemea ahadi na wakaacha bidii za kumwabudu. (Bukhaaree wa Muslim)

Yaliyo muhimu katika sura hii:

1. Hikma ya kuumbwa majini na wanadamu
2. Ibada ya Allaah ndiyo tawheed kwani kinyume chake ni shirk ambayo humbaidisha mtu na Allaah.
3. Yeyote asiyetekeleza masharti ya Tawheed, huyo hajamuabudu Allaah vilivyo,kwani ni katika Tawheed tu ndio hudhihirika maana ya ayah**:" Wala nyinyi hamuabudu Ninayemuabudu (109:3)**
4. Hikma ya kutumwa Mitume Alayhi muss-alaam.
5. Kwamba ujumbe wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) ni kwa watu wote ulimwenguni.
6. Mitume wote wametumwa na dini moja.
7. Muhimu Ibaada ya Allaah haikamiliki bila ya kuwakanusha na kujiepusha na mataaghuti. Na hapo ndipo penye maana ya ayah **-Basi anayemkufuru *Tâghût* [1] na akamwamini Allaah, bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika.** (**Soorah al-Baqarah, 2:256)**
8. Kwa ujumlani Taaghut ni chochote kinacho abudiwa kinyume na Allaah.
9. Kwamba waumini wakweli wameutambua umuhimu mkubwa wa aya hizi tatu za sutaul An-'am (6:151-153) ambazo pia zajumuisha mambo mengine kumi,na ya kwanza ni kukemea shirk.
10. Ayah bayana za suratul Isra,ambazo ni ayah ya 22 hadi 39 zashughulikia mas-ala kumi na nane Humo ameanza Allaah kwa kauli yake –

لَّا تَجۡعَلۡ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَتَقۡعُدَ مَذۡمُومٗا مَّخۡذُولٗا ﴿٢٢﴾

Usimfanye mungu mwengine pamoja na Allaah, usije ukawa wa kulaumiwa uliye tupika (Soorah al-Isra' 17:22)

وَلَا تَجْعَلْ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَتُلْقَىٰ فِى جَهَنَّمَ مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٩﴾

Wala usimweke pamoja na Allaah - mungu mwengine, usije ukatupwa katika Jahannamu ukilaumiwa na kufukuzwa (Soorah al-Isra' 17:39)

ذَٰلِكَ مِمَّآ أَوْحَىٰٓ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ ٱلْحِكْمَةِ ۗ

Haya ni katika hikima alizo kufunulia Mola wako Mlezi (Soorah al-Isra' 17:39)

11. Maana ya ile aya katika suratun Nisa ijulikanayo kama ayah ya nyajibu kumi za binadamu, ambayo yaanza kwa:

وَٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ شَيْـًٔا ۖ

Muabuduni Allaah wala msimshirikishe na chochote (Soorah an-Nisa' 4:36)

12. Tanbihi juu ya wasia wa mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) wakati wa kufariki kwake .
13. Kuzijua haki za Allaah juu yetu.
14. Kujua haki zetu kwa Allaah pindi tukitekeleza nyajibu zetu kwake.
15. Tatizo hili la mwisho si lenye kujulikana kwa wengi miongoni mwa Maswahaba (Radhiallaahu 'anhum)
16. Ruhusa ya kubakisha jambo hili kuwa ni siri ili waja wajitahidi zaidi kumwabudu Allaah .

17. Ubora wa kumbashiria muislamu yamfurahishayo.
18. Khofu ya kutegemea ukubwa wa Rehma ya Allaah**.**
19. Jibu la aulizwaye kukhusu asoyajua: **"Allaah na Mtume wake ndio wajuao Zaidi "**
20. Uwezekano wa kupewa elimu baadhi ya watu bila ya wengine.
21. Tawadhui yake Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) hadi ya kupanda punda tena pamoja na mtu mwengine.
22. Kujuzu watu wawili kupanda mnyama mmoja.
23. Fadhila za Mu'aadh ibn Jabal (Radhiallaahu 'anhu)
24. Umuhimu Wa Jambo hili la **Tawheed**.

<u>Kumbukumbu</u>

[1]- Maana ya neno *Tâghût* ni pana sana: Lina maana ya kitu chochote kinachoabudiwa kinyume cha **Allaah**, yaani: viungu vyote visivyokuwa Allaah. Wanaweza kuwa ni Mashetani, Majini, Masanamu, Mawe, Jua, Nyota, Malaika na Wana-adamu. Mara nyengine *Tâghût* ina maana ya Hakimu mpotofu anaehukumu kwa njia isiyokuwa ya sawa. (An-Nisa 4:60) [Angalia Tafsir ya Ibn Kathir, na V.4:51] -- lakini Mtu anaye abudiwa kinyume na matakwa yake na yeye haridhiki na huko kuabudiwa na wala haja amrisha watu wamuabudu basi yeye hasemekani kuwa ni taaghoot. **THE NOBLE QUR'AAN**

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Shaykh ul Islaam Ibn ul Qayim alisema - ***At-Tâghût*** ni mtu yoyote anaetukuzwa na kuenziwa kuliko anavyostahiki?, Kama ni mtu anaeabudiwa, anaefanyiwa utiifu, au anaeandamwa.

Shaykh Muhammad in Abdulwahhaab alisema **Tâghût** ni wengi na viongozi wao ni watano: (1) Iblees, Laana ya Allaah imshukie; (2) Kila anaeabudiwa na akaridhika na hilo; (3) Kila anaelingania watu wamuabudu yeye; (4) Kila anaedai yakwamba anamiliki chochote katika ilimu ya mambo yaliyofichamana na mambo ya siri (al ghayb); (5) Na yoyote anaehukumu kwa yasiyokuwa yale Aliyoyateremsha Allaah.